# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA TATU

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA

**26 MEI, 2016**

**MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**TAREHE 26 MEI, 2016**

## I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

**Makatibu Mezani**

1. Ndg. Theonest Ruhilabake
2. Ndg. Neema Msangi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

1. Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

2. Mhe. Hussein Mohamed Bashe aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/17.

3. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf – Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi aliwasiisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

## III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na.239 – Mhe. Moshi Selemani Kakoso
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Moshi Selemani Kakoso
(ii) Mhe. Grace Sindato Kiwelu
(iii) Mhe. Ally Keissy Mohamed

Swali Na.240 – Mhe. Hussein Mohammed Bashe
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Hussein Mohammed Bashe

(ii) Mhe. Pauline Philipo Gekul
(iii) Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu

Swali Na.241 – Mhe. Esther Nicholas Matiko
Swali la nyongeza: Mhe. Esther Nicholas Matiko

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**
Swali Na.242 – Mhe. Neema William Mgaya
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Neema William Mgaya
(ii) Mhe. Qambalo Willy Qulwi
(iii) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**
Swali Na.243 – Mhe. Sixtus R. Mapunda [kny. Mhe. Janeth Mbene].
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Janeth Zebedayo Mbene
(ii) Mhe. Ester Michael Mmasi

Swali Na.244 – Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko
Swali la nyongeza: Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**
Swali Na.245 – Mhe. Riziki Shahari Mngwali
Swali la nyongeza: Mhe. (i) Mhe. Riziki Shahari Mngwali
(ii) Mhe. Ali Salim Ali

Swali Na.246 – Mhe. Elias John Kwandikwa
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Elias John Kwandikwa
(ii) Mhe. Abdallah Hamisi Ulega

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**
Swali Na.247 – Mhe. Faida Mohammed Bakary kny Mhe. Tauhida C. Gallos
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Faida Mohammed Bakary
(ii) Mhe. Tauhida Cassian Gallos

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:**
Swali Na.248 – Mhe. Cecilia Daniel Paresso
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Cecilia D. Paresso
(ii) Mhe. Abdallah H. Ulega

## IV. MATANGAZO:

1. Wageni wote waliokuwepo Ukumbini walitambulishwa.

2. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo aliwatangazia Wajumbe wake wakutane saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa D.

3. Wabunge wote walitangaziwa kuwa kesho tarehe 27.5.2016 kutakuwepo na Warsha kwa Wabunge wote kuhusu Magonjwa yasiyoambukizwa, saa 7.30 hivyo wanaombwa kuhudhuria katika ukumbi wa Msekwa.

4. Wabunge wote walitangaziwa kuhusu upimaji wa hiari juu ya afya zao katika Zahanati ya Bunge. Na huduma hiyo ni bure. Aidha huduma hiyo itakuwa siku ya Jumamosi tarehe 28 Mei, 2016.

5. Katibu wa Wabunge wa wa CCM aliwatangazia Wabunge Wanawake kuwa leo tarehe 26/5/2016 wakutane katika ukumbi wa Msekwa saa 7.00 mchana.

**MAJIBU YA MWONGOZO WA MHE. ESTHER NICHOLAS MATIKO**

- Naibu Spika alitoa nafasi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili aweze kujibu Mwongozo uliotolewa na Mhe. Esther Matiko kwani mwongozo huo ulikuja kama swali, kwamba Posho ya Askari Magereza huchelewa kutolewa sana.

  Waziri alijibu sababu za ucheleweshaji huo kuwa ni kupanda kwa posho hiyo kutoka sh.180, 000 hadi 300,000 na hivyo kusababisha marekebisho hayo kuchukua muda. Pia alisema posho hiyo imeshapelekwa Benki, hivyo watapata baada ya muda mfupi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

- Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo kuwa, kwa kuwa imeonesha kuwa Bunge kutooneshwa live ni Hatari, Waziri wa Habari (Mhe. Nape Nnnauye) alizomewa katika Tamasha la Muziki jambo linaloweza kuendelea kwa Waziri Mkuu na Mawaziri wengine kuweza kuzomewa, ni kwanini Bunge live isirudishwe kwenye TBC1?

- Mhe. Esther Matiko alitumia Kanuni ya 68(7) akashukuru kwa majibu ya Waziri na kusema majibu hayakuwa sahihi kwani Askari wamechelewa sana kulipwa na posho ya pango ilizuiliwa na bado haijaanza kulipwa.

**MAJIBU YA NAIBU SPIKA**

Naibu Spika aliwakumbusha Wabunge Matumizi Mazuri ya kanuni ya 68(7) kwamba, Kanuni hii inahusu jambo lililotokea mapema Bungeni". Hivyo Mbunge aombapo mwongozo jambo hilo liwe limetokea Buneni na aulize kama linaruhusiwa au la. Vinginevyo Wabunge watumie kanuni nyingine zinazotoa fursa mbalimbali zinazoweza kukidhi hoja ya Mbunge.

Aidha, alimwomba Mhe. Esther Nicholas Matiko alete ushahidi wake kuonesha uongo wa majibu ya Mheshimiwa Waziri ili kuweza kulinganisha na kiti kitoe Mwongozo sahihi.

Akimjibu Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi Mwongozo wake, Naibu Spika alisema Tamasha la Muziki halijatokea Bungeni mapema, hivyo Kanuni ya Mwongozo haihusiki. Mhe. Mbilinyi anawez akutumia kanuni nyingine kuleta hoja yake.

**V. HOJA ZA SERIKALI**

Hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na ufundi kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/17.

Mjadala ulianza baada ya Hoja hiyo kuwasilishwa kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Hussein Mohamed Bashe
2) Mhe. Suzan Anselm Lyimo

**MWONGOZO**

1) Mhe. Angellah Jasmine Kairuki – Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, alitumia kanuni ya 68(7) kwamba yote yaliyozungumzwa na Msemaji wa Upinznai katika ukurasa wa 2 na 3 siyo ya kweli kwnai ni ukiukwaji mkubwa wa kanuni kusema kuwa CCM ilipata ushindi wa kuchekechwa wakati ushindi ulikuwa zaidi ya asiimia 70 na matokeo yalikuwa halali.

2) Mhe. Amina Saleh Mollel alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo pamoja na Ibara ya (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia kitendo cha mtu na mkewe kuuawa kwa kukatwa na mapanga. Je, nini wajibu wa Serikali katika kuhakikisha raia wanaishi kwa amani?

3) Mhe. Nape Moses Nnauye alisema kuwa Mwongozo uliotolewa na Mhe. Joseph Mbilinyi hauna ukweli wowote.

Uchangiaji uliendelea kama ifuatavyo:-

4) Mhe. Mary Chatanda - CCM
5) Mhe. Juma Nkamia - CCM

**MAJIBU YA MWONGOZO**

- Naibu Spika alijibu Mwongozo wa Mhe. Nape Nnauye kuwa Maneno ya Mhe. Joseph Mbilinyi yalikataliwa kuwa mwongozo basi na hoja yake inakufa.

- Hoja ya Mhe. Amina Saleh Mollel, kuwa Serikali ifuatilie kwa karibu ili jambo hili likomeshwe. Pia alielekeza kuwa jambo hili liletwe katika utaratibu mwingine.

- Kuhusu Mwongozo wa Mhe. Angellah Kairuki ni kwamba, kulikuwa na uchekechwaji wa matokeo, ukurasa 4, sentensi ya mwisho – Serikali imeanza kuingilia hotuba za Upinzani na kuifanya Sensorship kuiondoa mezani Hotuba tarehe 26/4/2016 ni kinyume na taratibu. Kamati ya kanuni iliagizwa kukutana ilete mapendekezo yake yasomwe Bungeni. kanuni ya 5(1) ipo iliyowekwa mara tatu na Kamati ya Kanuni ilikaa – aliagiza kuanza ukurasa 2-4 yale yaliyo kinyume na kanuni yaondolewe.

**VI. KUSITISHA BUNGE**

Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

**VII. BUNGE KUREJEA**

- Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na mwenyekiti, Mhe. Andrew John Chenge. Majadiliano ya Hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi yaliendelea kama ifuatavyo:-

3. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga - CCM
4. Mhe. Esther Michael Mmasi - CCM
5. Mhe. Juliana Daniel Shonza - CCM
6. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola - CCM
7. Mhe. Dkt. Elly Marco Macha - CHADEMA
8. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf - CUF
9. Mhe. Silafu Jumbe Maufi - CCM
10. Mhe. Dkt.Elias Hassan Masala - CCM
11. Mhe. Halima Abdallah Bulembo - CHADEMA
12. Mhe. Pauline Philopo Gekul - CHADEMA
13. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru - CHADEMA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki | - | CCM |
| 15. | Mhe. Bonnah Moses Kaluwa | - | CCM |
| 16. | Mhe. Ester Alexander Mahawe | - | CCM |
| 17. | Mhe. Mwanne Ismael Mchemba | - | CCM |
| 18. | Mhe. Yussuf Kaiza Makame | - | CUF |
| 19. | Mhe. Zainab Musa Bakari | - | CHADEMA |
| 20. | Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa | - | CCM |
| 21. | Mhe. Deogratias Francis Ngalawa | - | CCM |
| 22. | Mhe. Sebastian Simon Kapufi | - | CCM |
| 23. | Mhe. Daniel Nsanzugwanko | - | CCM |
| 24. | Mhe. Jesca David Kishoa | - | CHADEMA |
| 25. | Mhe. Abdallah Nachuma Maftaha | - | CUF |
| 26. | Mhe. Pascal Yohana Haonga | - | CHADEMA |
| 27. | Mhe. Phillip Augustino Mulugo | - | CCM |
| 28. | Mhe. Rashid Mohamed Chuachua | - | CCM |
| 29. | Mhe. Edward Franz Mwalongo | - | CCM |

**VIII. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 27/5/2016 saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA**
**26 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**